

MTIHANI WA PAMOJA NYAHOKAKIRA 2024

Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

(LUGHA)

Julai 2024 - Muda: Saa 2 Dakika 30

Jina: Nambari:

Mkondo..... Shule.....

Maagizo

- Andika jina lako na namba yako ya usajili, mkondo na jina la shule katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali yote.
- Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
- Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.
- Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

Siku hiyo kituo cha magari ya usafiri wa umma kilikuwa kimesongamana abiria kila mmoja akisaka fursa ya kuabiri chochote kinachoweza kuendeshwa walau afike nyumbani- mashambani hasa, ili kujumuika na wapendwa wake kusherehekea pamoja wakati wa kipindi cha tamasha nyingi. Kila gari lilipofika lilikimbiliwa na kuwaniwa kama mpira wa kona chambelecho watangazaji wa mpira. Kwa hakika kukimbia hakukuwa mzigo mzito kama ule wa kuabiri gari lenyewe na kupata kiti cha kukalia pindi walipolifikia. Waliobahatika kuwa na ubingwa wa kiriadha walisalitiwa na jinsi, umri, uzito wa mizigo waliyosheheni migongoni na mabegani. Aghalabu wale wa jinsia ya kiume, wakubwa, waliokuwa na miraba mine bila mizigo au mizigo miepesi waliwapiku wenzao waliokuwa vinginevyo. Kwa kweli katika hali hii, wengi walikumbatia purukushani; uungwana ulikuwa mbali sana na waja. Walioshindwa kuabiri walilazimika kusubiri magari mengine yafike. Ingawa mimi nilijaliwa sifa nyingi zilizowawezesha abiria wenzangu waliowania nafasi katika vyombo vya kusafiria, na ningeweza kijiingiza katika mkumbo huo, malezi yangu yalinizuia kujitoma kwenye kinyang'anyiro hiki. Nilielewa kwamba waso haya wana mji wao. Huo haukuwa mji wangu kamwe.

Nilibaki nimeduwaa pale penye kibanda cha kujizuia jua nikisubiri zamu yangu ama sijui gari langu. Kisha mawazo yakaanza kunipitikia mfululizo; naam maswali ya balagha kama wanafasihi wayaitavyo. Mbona serikali isiandae taratibu za usafiri wa umma wakati wa shughuli nyingi za usafiri wa watu kama vile sherehe, ufunguzi na ufungaji wa shule? Na kama itaandaa taratibu hizi, je ni wangapi miongoni mwetu watazifuata madhali watu wengi wanapenda ama kupuuza au kukaidi serikali na mipango yake hata pale ambapo ni maslahi yao yanadhamiriwa kulindwa? Aidha, si utepetevu wa wanaotakiwa kusimamia taratibu zenyewe utaingilia na kuhujumu malengo yake? Nilipokuwa naendelea kuwaza hivi, ikasadifu kwamba, sumba, rafiki yangu na jirani kijijini kwetu, na ambaye niliandamana naye katika safari ya kwenda kwetu Manda, akanikumbusha kwamba kulikuwa na wakati ambapo yalikuwepo magari ya usafiri wa umma yaliyomilikiwa na serikali.

Ndipo mawazo yangu yakarejea katika miaka hiyo awali. Nikakumbuka nikisafiria magari haya nikienda katika shule kwa masomo yangu ya upili. Kulikuwa na ratiba iliyofuatwa kikamilifu na magari haya na tulijua vyema. Wasafiri wangetabiri saa za kuwasili pale walipokuwa wanaenda na hata kuwaambia wapendwa wao wawasubiri kwenye vituo vya mabasi vya huko waendako. Kumbuka siku hizo rununu hazikuwepo na watu walitegemea simu za 'kurogaroga' kama watu walivyozoea kuziita-zile za kutumbukizwa sarafu kwenye kijitaro kilichoelekeza sarafu katika kisanduku kilichokusanya safari hizo ili zichukuliwe na maafisa wa Shirika la Posta na Simu zijaapo. Simu zenyewe zilikuwa zimejengewa vibanda ili kuzisetiri dhidi ya jua na mvua. Waliopiga simu walikuwa na siri zao ambazo zingesikilizwa na wasiodhamiriwa laity hakungekuwa na vibanda hivi.

Basi turejee palepale pa zamani – **zamani yenye thamani**. Umakinifu wa madereva walioendesha magari hayo pamoja na uraifu na ungwana wa maafisa wengine waliohudumu huko kama utingo na wahasibu, ni mambo niliyokosa kila niliposafiria magari ya watu nay a kampuni za kibinafsi. Ajali hazikutokea hiholela na kwa muda sikuelewa sababu hadi babu aliponiambia kuwa madereva wa hayo magari haya alikuwa ametoka katika shirika hili lililjulikana kwa kuisitiza nidhamu ya kiwango cha juu miongoni mwa vijana waliosomea huko. **Vimondo** baina yao baada ya malipo, kushukishwa mbele au waliotumia magari yaliyomilikiwa na serikali.

Siku hiyo nilipokuwa ninashuhudia mahangaiko tuliyokuwa tunapitia, nilijiuliza ni nini kilichosambaratisha mpango huo mzuri wa usafiri wa umma. Bila shaka lilikuwa zao la ulegevu wa usimamizi. Namkumbuka babu akinieleza kwa masikkitiko makubwa, miaka michache baadaye kwamba wasimamizi walipuuza hitajio la ukarabati wa mara kwa mara wa magari haya licha ya kuhitajika kutengwa fedha za kufanyia shughuli hii. Pesa zenyewe zilielekezwa kwenye mifuko ya watu binafsi. Hii chovya chovya ilipigisha magoti shirika hili na hatimaye ikamaliza buyu la asali. Nilipokumbuka hali ilivyokuwa miaka hiyo nikahofia kwamba hata kama serikali itaanzisha mpango kama huu tena, suluhisho halitakuwepo kwa sababu ubadhirifu wa mali ya umma **umeshitadi** zaidi wakati huu kuliko ulivyokuwa siku hizo na hasa wakati huu ambapo maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia ni makubwa zaidi.

Tulikaa kibandani tukisubiri gari la kwenda kwetu kwa zaidi ya saa kumi. Ilipotimia saa kumi na moja tulighairi nia na kuahirisha safari yetu siku ambayo ingefuata. Tuliona kuwa ilikuwa bora kuchelewa na kufikia salama na siha zetu kuliko kupapia kwenda kwa namna yoyote ile halafu tuishie kujuta. Asubuhi iliyofuata rafiki yangu Dokta alitupa lifti katika gari lake na kutuwezesha kujiunga na ila yetu ya mashambani ili kusherehekea sikukuu ya mwaka mpya pamoja. Watu wengi wenye magari ya kibinafsi hawakuwa wepesi wa kuwaauni wenzao ambao hawakujaliwa kuwa na magari hasa katika kipindi chenye msongamano wa abiria kama hiki lakini Dokta alikuwa tofauti sana.

Maswali

- a) Taja mambo **matatu** yaliyowazuia abiria waliokuwa hodari katika riadha kuabiri magari kwa urahisi. (al. 3)

.....

.....

.....

- b) Rejelea mambo mawili yanayomwonyesha msimulizi kuwa mtu mwenye hekima. (al. 2)

.....

.....

- c) Msimulizi anasema ‘zamani ya thamani’. Kwa kurejelea matukio matano katika kifungu. Thibitisha ukweli wa kauli hii. (al. 5)

.....

.....

.....

.....

.....

d) Taja majukumu mawili yaliyotekelezwa na vibanda vilivyojengewa simu. (al. 2)

.....
.....

e) *Matatizo ya usafiri* ni kichwa mwafaka kwa makala haya. Pendekeza kichwa kingine kinachofaa makala haya. (al. 1)

.....

f) Eleza maana za maneno yafuatayo katika muktadha wa makala uliyosoma. (al. 2)

i) Vimondo

ii) Umeshitadi

UFUPISHO (ALAMA 15)

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya sasa baada ya uhuru, bali ni matokeo ya hali iliyokuepo tangu enzi la mababu zetu; kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kiasi kunapana na kuonyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa siku nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi ilimwandaa mwanamke kuwa chocmbo kitiifu cha mwanamume. Mwanamke aliandaliwa katika unago na katika mfumo mzima wa malezi kuwa chombo cha kutumikia mwanamume-kumstarehesha, kumfariji, kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angeweza kushikilia wadhiu wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi naihusudu sana; ambapo wazee walikaa chini ya kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya kijiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwanamke aliyeshirikishwa, hata kama alikua ajaza. Sifa waliokuwa nayo wanawake ni ile ya usihiri na uganga. Mwanamke yeyote aliyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa wa uchawi, ulozi na ushirikina. Kwa hivyo, wanawake ndio waliokuwa washirikina wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwaname alipojitokeza na kusema jambo la busara, aliuupza na pengine kutukanwa hadharani.

Kwa bahati nzuri, kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzu mpya. Vita vya wanawake vya kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia. Wanawake weni wamekiuka misingi na mizizi ya utamaduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kumnyanyasa na kumuumbua utu mwanamke tangu jadi. Watetezi wa haki za wanawake zamani walilaumu suala la serikali za mataifa mwaka hadi mwaka. Huku maswala ya wanawake ya kijamii, uut na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa, watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nchi moja. Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengi yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, kusiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa, na ushirikiano wa kimataifa, majukumu yao katika jamii, mfukowa umoja wa Mataifa wa wanawake (Unifem) na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya Umoja wa Mataifa mlongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu.

Wanawake wameonyesha vipaji vya katika Nyanja mbalimbali za maisha; siasa, uchumi, utawala na kadhalika. Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wanajukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na ya watu wengi. Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kuukubali ukweli huu, wapende wasipende. Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja nay a wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi, wapinga mila na watovu wa utii.

Maswali

a) Bila kubadilisha maana asilia, fupisha aya tatu za kwanza (Maneno 45-55) (al. 6)

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Jibu

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

b) Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, pambanua hoja muhimu zinazoguziwa na mwandishi (Maneno 60 – 65) (al. 9)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- a) **i)** Andika neno lenye muundo wa sauti zifuatazo kuzuio-kwamizo sikhuna, irabu ya nyuma kati, kimadende, irabu ya chini. (al. 1)

.....
.....

- ii)** Tofautisha irabu za juu. (al. 1)

.....
.....

- b) Onyesha miundo ya silabi katika neon; (al. 2)
nyoosha

.....
.....

- c) Tunga sentensi moja katika wakati ujao yenye vitenzi vishirikishi sambamba. (al. 2)

.....
.....

- d) Ainisha mofimo katika maneno yafuatayo. (al. 2)
i) Alaye

.....
.....

- ii) Mtu

.....
.....

- e) Andika katika wingi. (al. 1)
Uliko ndiko kuliko nacho

.....
.....

- f) Andika sentensi ukitumia kivumishi kisisitizi cha mbali kidogo katika ngeli ya u-i, umoja. (al. 2)

.....
.....

- g) Kanusha (al. 3)
Tunda ambalo limeiva ni tamu

.....
.....

.....
.....

h) Tambua virai katika sentensi ifuatayo. (al. 3)
Insha nzuri iliandikwa vizuri na mwanafunzi mtiifu.

.....
.....
.....

i) Tambua kiima na yambiwa katika sentensi ifuatayo. (al. 2)
Mama aliandaliwa maandazi matamu na mwanawe kwa kikaango kipya juzi

.....
.....

j) Andika upya sentensi zifuatazo ukizingatia maagizo mabanoni. (al. 2)

i) Ubora wa kazi zao ulifichika kabla ya kuanzishwa kwa mradi ule (kinyume)

.....
.....

ii) Mhandisi alikarabati mtambo. (al. 2)
Mtambo ulikuwa kiwandani (unganisha bila kutumia kiunganishi)

.....
.....

k) Ainisha sentensi ifuatayo kiuamilifu na kimuundo.. (al. 2)
wageni walifika wakalakiwa vyema

i) Kiumalifu

.....
.....

ii) Kimuundo

.....
.....

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa mtindo wa Jedwali. (al. 4)
Mlango umevunjwa japo ulikuwa umefungwa kwa kufuli

.....
.....
.....
.....

m) Tambua maana zinazojitokeza katika sentensi zifuatazo. (al. 2)

i) Wangetembelea nchi nyingi wangepata maarifa mengi.

.....

ii) Wangalitembelea nchi nyingi wanalipata maarifa mengi

.....

n) Onyesha matumizi mawili ya alama za mtajo. (al. 2)

.....

.....

o) Andika katika usemi wa taarifa.

“Sitakwenda sokoni leo bali nitakwenda kesho” Nikamjibu

.....

.....

p) Bainisha matumizi ya kiambishi – li- katika utungo huu. (al. 3)

Alivyolikimbilia

.....

.....

.....

q) Andika katika ukubwa. (al. 2)

Maji ya kijito kile yalikusomba kitoto hicho kikafa

.....

.....

r) Andika methali moja inayoafiki muktadha huu. Baada ya Wanga kushindwa katika mtihani alidai kuwa walimu wake hawakuwa wamemwelekeza vizuri. (al. 1)

.....

.....

ISIMU JAMII 9ALAM 10)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujimbu maswali yanayofuata

“Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana kabla ya kujongea mezani pake Bwana, pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu.”

a) i) Bainisha sifa tatu za sajili zinazopatikana kwenye kifungu uliocosoma. (al. 3)

.....
.....
.....

ii) Tambua sifa tatu nyinginezo za sajili hii. (al. 3)

.....
.....
.....

b) wewe kama kiranja umeombwa kutoa ushauri kwa wenzako kuhusu umuhimu wa ushirikiano. Eleza sifa za lugha utakayotumia katika muktadha huu. (al. 4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....